

**OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA RORYA
SHULE YA SEKONDARI GORIBE**

S.L.P 313

TARIME – RORYA

KUMB.NO.GSS/MKSS/VOL

JINA LA MWANAFUNZI;

S.L.P

RORYA

**YAH; MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI GORIBE WILAYA YA RORYA,
MKOA WA MARA KWA MWAKA 2023.**

1.0 UTANGULIZI

Ninafurahi kukuariafu kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza mwakakatika shule ya sekondari Goribe, ambayo ipo umbali wa KMkaskazini mashariki ya Halmashauri ya wilaya ya Rorya.

Muhula wa kwanza wa masomo unaanza tarehe na unatakiwa kuripoti shulenii kuanzia tarehena mwisho wa kuripoti shuelini ni tarehe ambapo ni ndani ya wiki mbili (siku 14).

2.0 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA.

2.1 SARE ZA SHULE.

➤ WASICHANA

Sare za shule hii kwa wasichana n;

- sketi mbili aina ya tetron /cotton rangi ya right blue na nyeusi, weka mistari miwili meupe mbele ya sketi nyeusi
- weka mistari miwili ya kijana kwenye light blue
- marinda yawe ya kati (si madogo sana)
- sketi zote zivuke goti (ziwe ndefu)
- mashati mawili (2) aina ya tetron/ cotton meupe yenyenye mikono mifupi yawe na kola na mifuko ya kushoto
- viatu vya ngozi nyeusi jozi/Pair mbili (2), soksi nyeupe pair 2
- Tai rangi nyeusi (1), light blue (2) urefu wake usivuke kitovu
- Sweta (1) rangi ya blue kwa ajili ya baridi

➤ WAVULANA

- Mashati mawili (2) aina ya tetron /cotton rangi nyeupe yenyenye mikono mifupi yawe na kola na mifuko ya kushoto.
- Suruali mbili, moja nyeusi na nyingine light blue
- viatu vya ngozi nyeusi jozi/Pair mbili (2), soksi nyeusi pair 2
- Tai mbili nyeusi (1), light blue (2) urefu wa tai zote zisivuke mkanda wa suruali
- Sweta (1) rangi ya blue kwa ajili ya baridi
- Mikanda(2) meusi isiwe na kichwa kikubwa au mapambo mengine

2.2 SARE ZA MICHEZO

- WAVULANA; Bukuta ya Blue na Tshirt rangi ya Ugoro na raba za michezo (zitavaliwa wakati wa vipindi vya michezo)
- WASICHANA; Bukuta ya Blue na Tshirt rangi ya Ugoro na raba za michezo (zitavaliwa wakati wa vipindi vya michezo)

3.0 MAMBO MENGINE .

- Kalamu,madaftari 11 na mkebe wa hesabu (mathematical set)
- Mahitaji ya kibinadamu kama matibabu(bima)
- Vifaa vya usafi (fyekeo na dumu la maji lita 10)
- File 1 kwa ajili ya kutunzia taarifa zake

3.1 SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE

Shule inaiendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu ya Na.25 ya mwaka 1975 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na.10 ya mwaka 1995.Aidha inazingatia miongozo yote iliyotolewa na wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia yenyenye dhamana ya elimu nchini pamoja na Ofisi ya Rais (TAMISEMI) yenyenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa maswala ya elimu nchini.Hivyo mwanafunzi anapaswa kuizingatia yafuatayo;

- Heshima kwa viongozi,wazazi,wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla
- Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule
- Kutekeleza kwa umakini shughuli zozote utakazo pewa kwa mujibu wa kanuni na taratibu za shule
- Kufahamu mipaka ya shule na kuizingatia kikamilifu,kuiheshimu katika kipindi chote unapokuwepo ndani na nje shule
- Kutunza usafi wa mwili pamoja na mavazi
- Kutunza mali za UMMA

3.2 MAMBO YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA AU KUSIMAMISHWA SHULE

- a) Wizi
- b) Uasharati na ushoga
- c) Ubakaji
- d) Ulevi na matumizi ya dawa za kulevya kama vile; uvutaji bangi, cocaine,sigara,mirungi n.k
- e) Kupigana au kupiga
- f) Kuharibu kwa makusudi mali ya UMMA
- g) Kudharau bendera ya Taifa
- h) Kugoma, kuchochea,kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa jamii ya shule kwa ujumla
- i) Kukataa adhabu kwa makusudi
- j) Kuwa na **simu** ya mkononi

4.0 MAELEZO MUHIMU (TANBIHI)

Siku ya kuja kuripoti shulenii,pamoja na fomu hii pia unapaswa kuja na fomu maaluma ya uthibitisho wa afya ya mwanao ikiwa imejazwa na mganga wa hospitali ya serikali inayotambulika

Unatakiwa wewe kama mzazi /mlezi wa mwanafunzi uwe umeisoma na kuilewaa vyema sheria za shule na kanuni zake na kujaza fomu hii na kuikabidhi siku mwanafunzi anaripoti shulenii ukiwa umeongozana nae. Siku ya kufungua shule ni tarehe na ifikapo tarehe.....ni mwisho wa kuripoti.

5.0 SEHEMU YA MWANAFUNZI

Mimi (jina) ambaye nimechaguliwa kujeungaa na masomo
katika shule ya sekondari Goribe kwa mwaka wa masomonaahidi/nakiri kuwa nimeisoma

na kuielewa vyema sheria na kanuni za shule na ninakubali kufuata sheria na kanuni hizo siku zote za uanafunzi wangu.

SAHIHI YA MWANAFUNZI.....

JINA LA MWANAFUNZI.....

6.0 SEHEMU YA MZAZI/MLEZI

Mimi mzazi/mlezi wa (jina la mwanafunzi) naahidi kumlea mwanangu kulingana na sheria na kanuni za shule na pia naahidi kushiriana na walimu katika kumlea mwanangu kwa mujibu wa kanuni na sheria za shule.

SAHIHI YA MZAZI/MLEZI.....

JINA LA MZAZI/MLEZI.....

.....
Sahihi na muhuri wa mkuu wa shule